

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI,

SHULE YA SECONDARI IDUNDA, SLP 48 MAKAMBAKO .

TAREHE 11/12/2020

JINA LA MWANAFUNZI

.....  
**YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI  
IDUNDA,WILAYA YA MUFIMDI ,MKOA WA IRINGA MWAKA 2021**

#### **1.0 UTANGULIZI**

Ninapenda kutumia nafasi hii kukupa hongera kwa kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya **sekondari IDUNDA**. Shule ipo katika kijiji cha ikangamwani kata ya Idunda taarifa ya Malangali,wilaya ya Mufindi.

Hali ya hewa ni nzuri kwa masomo ,shule hii ni kutwa na niya mchanganyiko wa wavulana na wasichana.Shule hii inafundisha masomo yafuatayo;

Hisabati,Jiografia,Historia,Uraia,Biolojia,Kiswahili,Kiingereza,Fizikia,Kemia.

#### **2.0 KUFUNGUA SHULE**

Shule itafungua tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shulen i kuanzia tarehe 11/01/2021 ukiwa na mahitaji yote ulioagizwa.

#### **3.0 VIFAA VYA TAALUMA**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo;

- Daftari 10 counter book
- Peni ya bluu au nyeusi
- Kalamu ya mkaa (pencil)
- Rula
- Mfuko wa kubebbe Daftari (BEGI)
- Dictionary 1 (English to English)
- Mkebe mmoja.
- **FLATE FAILI MOJA** kwa ajili kutunzia kumbukumbu zake.

#### **4.0 SARE YA SHULE**

##### **➤ WAVULANA**

- 1.suruali mbili ,moja ya kijani na nyingine ya kijivu mpauko.
- 2.shati nyeupe mbili,moja mikono mifupi na nyingine mikono mirefu.
- 3.viatu vya ngozi vya kamba jozi 2 rangi nyeusi.(boot haziruhusiwi kabisa)
- 4.soksi jozi 2 rangi nyeupe

**5.sweta mbili ,moja ya kijani na nyingine ya kijivu mpauko**

**6. Tai 2 ,moja ya kijani na nyingine ya kijivu mpauko**

➤ **WASICHANA**

1.Sketi mbili,moja ya kijani na nyingine ya kijivu mpauko (Estem no 1)

2.Shati nyeupe 2, moja mikono mirefu na nyingine mikonomifupi

3.viatu nya ngozi nya kamba jazi 2 rangi nyeusi.(**boot haziruhusiwi kabisa**)

4.soksi jazi 2 rangi nyeupe

**5.sweta mbili ,moja ya kijani na nyingine ya kijivu mpauko**

**6. Tai 2 ,moja ya kijani na nyingine ya kijivu mpauko**

**NB: kila mwanafunzi ashone sare kwa kuzingatia rangi na aina ya kitambaa alichoelekezwa na zenye maadili.**

## **5.0 SARE ZA MICHEZO**

- Tracksuit jazi moja rangi ya bluu
- Tshirt ya njano moja au zaidi
- Raba /viateu nya michezo

## **6.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na.10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu sayansi na Teknolojia na Ufundu yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye usimamizi wa uendeshaji wa Elimu.unatakiwa kuzingatia mambo ya fuatayo kipindi chote cha uanafunzi wako

- Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,na wanafunzi wenizio
- Mahudhurio mazuri kila siku kwa kuzingatia ratiba ya shule
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingztia kikamilifu maelekekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wowote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule
- Kuvalaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- Kuzingatia ratiba ya shule wote
- Kutunza mali za umma

### **6.1 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

- Wizi
- Uasherati

- Ubakaji
- Ulevi wa pombe, uvuataji bangi na madawa ya kulevya
- Kupiga au kupigana
- Makosa ya jinai
- Kudharau au kuharibu bendera ya Taifa
- Kupata mimba au kusababisha mimba
- Kutoa mimba
- Kukataa adhabu kwa makusudi
- Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- Kuwa na simu ya mkononi
- Kuoa au kuolewa
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

## **6.2 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI ANAPORIPOTI MWANAFUNZI**

- Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali
- Fomu ya tamko la mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

**NB:soma kwa makini maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SANA IDUNDA SEKONDARI**

.....  
**ELIARD S. MAHALI**  
**MKUU WA SHULE**